# GPSA yajivunia mafanikio lukuki miaka minne ya uongozi wa Rais Samia

Maliki Muunguja, Mwananchi




**Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Wizara (MAB), Bi. Dorothy Mwanyika (kulia) na Afisa Mtendaji Mkuu wa GPSA, Profesa Geraldine Rasheli (kushoto) baada ya kutunikiwa tuzo kwa kudhamini Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki lililofanyika Septemba 9-12, 2024 Jijini Arusha.**

Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) ni miongoni mwa taasisi za umma zinazojivunia mafanikio makubwa katika kipindi cha Serikali ya awamu ya sita ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk Samia Suluhu Hassan.

GPSA ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya mwaka 1997 na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 235 la Desemba 7, 2007. Aidha katika Sheria hiyo, kulifanyika marekebisho kupitia Gazeti la Serikali Na. 133 la Aprili, 13, mwaka 2012.

Kuanzishwa kwa GPSA ni matokeo ya programu za uboreshaji wa utendaji katika sekta ya umma ambapo iliyokuwa 'Bohari Kuu ya Serikali' ilifutwa na baadhi ya majukumu yake yalichukuliwa na GPSA ambayo uzinduzi wake ulifanyika rasmi Juni 16, 2008. GPSA iko chini ya Wizara ya Fedha, ikiwa na ofisi na vituo vya mafuta katika mikoa yote na baadhi ya wilaya za Tanzania Bara.

GPSA ni kitovu cha ubora katika mnyororo wa usimamizi wa ugavi nchini wenye kuzingatia thamani halisi ya fedha, ikijivunia kuacha alama katika muhula wa kwanza wa uongozi wa Rais Samia.

### Makusanyo ya Serikali

Afisa Mtendaji Mkuu wa GPSA, Profesa Geraldine Rasheli anasema kuwa GPSA inajivunia kuwa miongoni mwa taasisi zilizochangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo imetoa zaidi ya Sh 16.27 bilioni kuanzia Julai, 2020 mpaka Desemba, 2024. Mchango huo umeendelea kuipaisha Tanzania kiuchumi kuifanya kuwa miongoni mwa nchi za Afrika zinazokuza uchumi wake kwa kasi.

Kama hiyo haitoshi, katika awamu hii ya sita, GPSA ilijiunga katika mfumo wa ununuzi wa mafuta kwa pamoja (Fuel Bulk Procurement) ambapo iliagiza mafuta yake kutoka nje ya nchi, mzigo wa kwanza mwezi Machi, 2024 ambapo imesaidia Serikali kuokoa fedha na ziada kutumika kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### Mageuzi ya kidijitali

Kwa mara ya kwanza katika Serikali ya awamu ya sita ya Rais Samia, GPSA inatoa huduma zake kwa njia ya mfumo wa kielektroniki wa GPSA Integrated Management Information System (GIMIS), uliotengenezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na kuzinduliwa rasmi Oktoba 21, 2023 na Dk Mwigulu Nchemba (Mb), Waziri wa Fedha, pamoja na majengo mapya yenye ofisi na vituo vya mafuta (Simiyu, Pwani, Songwe na Mtumba-Dodoma) jijini Dodoma. Aidha, mfumo wa GIMIS utaunganishwa na malipo na mifumo mingine ya Serikali ('single window') ikiwemo Mfumo wa Ununuzi wa Umma wa NeST.

Profesa Rasheli anasema mfumo huu unawezesha taasisi za umma kupata huduma zote za GPSA kidijitali kwa kutumia simu na kompyuta.

"Kupitia mfumo huu wateja wanapata orodha na bei ya vifaa vinavyopatikana, kufanya malipo na kupata stakabadhi na kisha kupata huduma katika vituo vyetu vilivyoko Mikoa yote 26 na Wilaya tatu. Pia kupitia mfumo huu wateja wanapata taarifa mbalimbali ikiwemo fedha na mwenendo wa matumizi yake kwa muda wowote," anaeleza zaidi.

Afisa Mtendaji Mkuu anabainisha: "GPSA ni taasisi ya kimkakati ya Serikali ikiwa miongoni mwa taasisi katika sekta ya ununuzi wa umma, ambapo sekta hii inakadiriwa kuwa na matumizi zaidi ya asilimia 70 ya bajeti ya Serikali, hivyo maboresho ya utoaji wa huduma zake kidijitali ni mapinduzi makubwa katika sekta hii."

### Maboresho ya huduma

GPSA imeendelea kuboresha utoaji wa huduma zake ambapo kwa sasa inatoa huduma ya mafuta kwa saa 24 katika vituo vyake vya Kisasa (Dodoma) na Kinondoni (Dar es Salaam). Mpango wa GPSA ni kufikia vituo vyake vyote kutoa huduma kwa saa 24. Vilevile anaeleza kuwa GPSA inatoa huduma katika ngazi za wilaya za Kinondoni (Dar es Salaam), Kahama (Shinyanga), Mtumba (Dodoma) na Ileje (Songwe). Aidha, GPSA imeanzisha kituo cha miito cha huduma kwa mteja kupitia namba 0735005005 ambapo wateja wanapiga simu na kusikilizwa kila siku za kazi kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa.

### Uwajibikaji katika jamii

GPSA imekuwa ikishiriki katika shughuli za kijamii kusaidia makundi mbalimbali na maendeleo kwa ujumla ikiwemo kutoa msaada katika maafa ya maporomoko ya matope katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang, Mkoa wa Manyara Desemba, 2023 kwa kutoa msaada wa fedha taslimu pamoja na mafuta ya dizeli ili kusaidia uokoaji pamoja na kuondoa tope.

**Sh 16.27 bilioni**

**Mchango wa GPSA katika mapato ya Serikali kuanzia Julai, 2020 mpaka Desemba, 2024.**

GPSA ilitoa msaada kufuatia maafa ya kuporomoka kwa jengo Kariakoo jijini Dar es Salaam kwa kuchangia mafuta (petroli na dizeli) kusaidia magari na mitambo katika uokoaji pamoja na huduma za uhifadhi wa mali za waathirika.

GPSA imekuwa mdau mkubwa katika michezo kwa kuchangia fedha taslimu kwa ajili ya maandalizi ya timu za Taifa katika mashindano ya Kimataifa ikiwemo timu ya Taifa ya wanaume katika mashindano ya AFCON yaliyofanyika mwaka 2024 nchini Ivory Coast.

### Tuzo

GPSA ilipata tuzo za uandaaji hesabu kwa kuzingatia viwango vya kimataifa katika sekta ya umma (IPSAS) kutoka Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA), kwa kushika nafasi ya tatu kwa mwaka 2021. GPSA ilitunukiwa cheti cha Uandaaji Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Client Service Charter) wenye viwango bora mwaka 2023.

Aidha, GPSA ilitunukiwa tuzo ya udhamini na cheti katika Kongamano la 16 la Ununuzi wa Umma la Afrika Mashariki mwaka 2024 lililoandaliwa na PPRA jijini Arusha, Kongamano la 15 la Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi 2024 lililoandaliwa na PSPTB Jijini Arusha pamoja na Mkutano wa elimu kwa Umma (wasitiri) 2025 ulioandaliwa na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) Jijini Mbeya.

> **Kumuunga mkono Rais Samia kwenye matumizi ya nishati safi, GPSA imejipanga kuanzisha huduma ya gesi asilia (CNG-V) kwa magari ya Serikali katika vituo vyake vilivyopo nchi nzima ambapo awamu ya kwanza ya mradi itahusisha mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro.**
>
> Afisa Mtendaji Mkuu wa GPSA, Profesa Geraldine Rasheli

### Faida ya kutumia GPSA

Baadhi ya faida ya kutumia huduma za GPSA kwa Taasisi za Ununuzi ni pamoja na uwepo wa wataalamu waliobobea katika huduma zinazotolewa, usalama wa mizigo ya Serikali, usalama wa mafuta kwa ajili ya vyombo vya moto ikiwemo magari hali inayosaidia kupunguza gharama za matengezo na usalama wa abiria, pamoja na kuondoa mianya ya rushwa kwa kuimarishwa uwazi na matumizi ya mifumo.

Taasisi za Serikali zinaepuka urasimu wa mchakato wa ununuzi kwa kuwa GPSA inafanya kwa niaba yake, urahisi wa kupata taarifa kwa wakati, bidhaa bora na halisi (original) ambazo hazichakachuliwi, kuondoa tofauti kubwa ya bei ya vifaa na huduma baina ya Taasisi moja na nyingine.

Kwa taasisi binafsi, ni kurahisisha uratibu wa zabuni za Vifaa na Huduma Mtambuka (VHM) kupitia mikataba maalumu kwa kushirikiana na PPRA, pamoja na wazabuni wakubwa na wazalishaji wa ndani kwa kununua mahitaji kwa wingi (bulk procurement) ikiwemo chaki, 'greentags' n.k na hivyo kuongeza masoko na kukuza mapato yao na hivyo kuchangia Serikali kupitia utoaji huduma na kodi.

### Mipango ya baadaye

Profesa Rasheli anasema kuwa katika kumuunga mkono Rais Samia ambaye ni kinara wa matumizi ya nishati safi, GPSA imejipanga kuanzisha huduma ya gesi asilia (CNG-V) kwa magari ya Serikali katika vituo vyake vilivyopo nchi nzima ambapo awamu ya kwanza ya mradi itahusisha mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Morogoro.

Aidha, kutokana na majukumu yake ya kisheria na kihistoria, GPSA ina miundombinu katika mikoa yote Tanzania Bara ambayo itasaidia kuhakikisha kwamba mfumo wa usambazaji nishati unafika nchi nzima kwa urahisi na uhakika.

Rais Samia amekuwa balozi namba moja wa uhamasishaji matumizi ya nishati safi nchini. Itakumbukwa kuwa mwaka uliopita alizindua Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024-2034 utakaowezesha walau asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ifikapo 2034.

Mbali na hilo, GPSA ina mpango wa kusogeza huduma zake katika wilaya 15 za kimkakati ikiwemo Korogwe (Tanga), Mbarali (Mbeya), Bagamoyo (Pwani) na Masasi (Mtwara). Pia, kuboresha utoaji huduma za GPSA katika ngazi ya kimataifa hadi kupata cheti cha kimataifa cha ithibati ya utoaji huduma (ISO) na kuwezesha GPSA kusogeza huduma katika masoko yaliyoko nje ya nchi.

GPSA imepanga kuongeza mapato yatokanayo na huduma ya ugomboaji na uondoshaji mizigo kwa kufikia nchi zisizokuwa na bandari na kuanzisha bandari kavu (ICD) kuweza kuhifadhi shehena zitakazokuwa zinagombolewa.

Profesa Rasheli anaongeza kuwa mpango wao mwingine ni kuuboresha mfumo wa GIMIS katika utoaji wa huduma ikiwemo huduma ya mafuta ili kuwezesha wateja kujihudumia wenyewe (kwa kutumia kadi) hata baada ya muda wa kazi.

### Majukumu ya GPSA

- Huduma ya Ugomboaji mizigo bandarini viwanja vya ndege na mipakani;
- Kununua magari ya Serikali kupitia Mfumo wa Ununuzi wa Pamoja;
- Kununua, kutunza na kuuza vifaa vya ofisi na vya shule,
- Kutoa huduma ya mafuta kwa ajili ya mitambo na magari ya Taasisi za Serikali;